# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

***2016/17***

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2017**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## 2016/17

## GAVANA
## BENKI KUU YA TANZANIA

Februari 2017

# Utangulizi

Taarifa hii ya mapitio ya Tamko la Sera ya Fedha inatathmini mwenendo wa utekelezaji wa Sera ya Fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17 na kuainisha mwelekeo wa kisera ambao Benki Kuu inakusudia kuchukua katika kipindi kilichobakia cha mwaka wa fedha 2016/17.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2017, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2016, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2015. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kumechangiwa na ukuaji hafifu katika nchi zilizoendelea kiuchumi (*advanced economies*), pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea (*emerging market and developing economies*). Ukuaji hafifu wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea ulitokana na wasiwasi juu ya uwezekano wa mabadiliko ya sera za uchumi, kushuka kwa mahitaji katika soko la dunia pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa shughuli za uzalishaji. Ukuaji duni wa uchumi wa nchi za kusini mwa jangwa la Sahara ulisababishwa kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia, kushuka kwa mahitaji ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi, pamoja na hali ya ukame.

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kuongezeka kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2017, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 katika mwaka 2016. Ukuaji huu unatarajiwa kuchangiwa zaidi na uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea, kutokana na matarajio ya kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bei ya mafuta pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani. Ukuaji wa uchumi katika

nchi za kusini mwa jangwa la Sahara unatarajiwa kuongezeka kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia pamoja na mahitaji binafsi.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi umeonesha mwelekeo wa kuongezeka. Mfumuko wa bei uliongezeka nchini Marekani, Uingereza, nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (*European Union*), na China; na ulipungua nchini India. Kwa nchi zilizopo mashariki na kusini mwa bara la Afrika, wastani wa mfumuko wa bei uliongezeka kutokana na hali mbaya ya hewa iliyochangia uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula; hali iliyojitokeza kwa miaka kadhaa mfululizo katika nchi nyingi za Umoja wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2017, mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2017, kutoka wastani wa asilimia 0.7 mwaka 2016. Ongezeko hili linatokana na matarajio ya kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, kufuatia makubaliano baina ya nchi wanachama wa OPEC kuweka mpango wa kupunguza uzalishaji wa mafuta. Mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea unatarajiwa kubakia katika wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2017.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### Tanzania Bara

Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2016, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Kuimarika kwa miundombinu; uthabiti wa upatikanaji wa nishati ya umeme ambao ulichangia kuongezeka

kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma kwa jamii; uwekezaji katika utoaji wa huduma za simu za viganjani na mtandao (*internet*), pamoja na bei za mafuta kuendelea kuwa za chini katika soko la dunia kumechangia kwa kiasi kikubwa kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi. Ukuaji wa uchumi katika robo tatu za mwanzo za 2016 ulichangiwa zaidi na shughuli za usafirishaji na uhifadhi (*transport and storage*) ambazo zilichangia asilimia 15.4, zikifuatiwa na shughuli za ujenzi (asilimia 11.0), mawasiliano (asilimia 9.5), biashara ya jumla na rejareja (asilimia 9.0), na madini (asilimia 7.9).

Mfumuko wa bei umeendelea kubakia chini ya asilimia 10 katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, ukifikia asilimia 5.0 mwezi Desemba 2016, ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwezi Juni 2016. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati (*core inflation*) umeendelea kubakia chini ya asilimia 3.0 katika kipindi hicho. Kushuka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa zaidi na Utekelezaji thabiti wa sera ya fedha, usimamizi madhubuti wa sera ya ukusanyaji mapato ya serikali na matumizi (*fiscal consolidation*), utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani, na kushuka kwa bei za baadhi ya vyakula na nishati.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 8,065.2, kiasi ambacho kilikuwa ni asilimia 22.1 zaidi ya mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti hizo katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, kiasi hicho ni sawa na asilimia 96.0 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kwa sehemu kubwa kumetokana na jitihada zinazotekelezwa na serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), zenye lengo

la kuongeza ukusanyaji wa mapato nchini, pamoja na kuongezeka kwa mapato mengine yasiyotokana na kodi. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi ya serikali yaliyofanywa kupitia katika akaunti za serikali zilizoko Benki Kuu yalifikia shilingi bilioni 8,535.4, yakiwa ni sawa na asilimia 1.3 zaidi ya matumizi yaliyofanywa kutoka katika akaunti hizo katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2015/16. Matumizi ya serikali katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17 yalikuwa ni asilimia 95.0 ya makadirio. Katika kipindi hicho, shilingi bilioni 6,452.4 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambayo ni sawa na asilimia 2.3 chini ya matumizi ya kawaida katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, matumizi ya maendeleo katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17 yalikuwa ni shilingi bilioni 2,083.0, ambayo ni sawa na asilimia 14.7 zaidi ya matumizi ya maendeleo katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2015/16.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*) ilipungua kwa asilimia 33.2 na kufikia dola za Marekani milioni 1,000.4, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani 1,498.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Kupungua huko kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje kulichangiwa na kupungua kwa thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 4,325.6 mwishoni mwa mwezi Desemba 2016, ambazo zinatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.2. Wakati huo huo, rasilimali za fedha za kigeni za mabenki ya biashara zilifikia dola za Marekani milioni 768.2, wakati amana za fedha za kigeni zilizohifadhiwa na wakazi katika benki za biashara nchini zilifikia dola za Marekani milioni 2,870.8.

Deni la sekta ya umma lilipungua kwa dola za Marekani milioni 123.5, kutoka dola za Marekani milioni 18,619.1 mwezi Juni 2016 na kufikia dola za Marekani milioni 18,495.5 mwezi Desemba 2016. Katika kipindi hicho, deni la nje likijumuisha deni la sekta binafsi lilipungua kwa asilimia 1.1 na kufikia dola za Marekani milioni 16,986.2 mwishoni mwa mwezi Desemba 2016, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 17,180.9 mwishoni mwa mwezi Juni 2016. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la nje la Taifa yaliofanyika mwezi Novemba 2016, yanaonesha kwamba thamani halisi ya deni la nje ikilinganishwa na pato halisi la Taifa (*net present value*) ilifikia asilimia 19.9, ambayo ni chini ya ukomo uliowekwa kimataifa wa kiwango cha uhimilivu wa deni la nje cha asilimia 40.0. Hii inamaanisha kwamba deni la nje la Tanzania bado ni himilivu.

Deni la ndani la serikali liliongezeka kwa asilimia 4.5 hadi shilingi bilioni 10,468.2 mwezi Desemba 2016, kutoka shilingi bilioni 10,012.7 mwezi Juni 2016. Ongezeko hili lilitokana na uuzaji wa dhamana na hati fungani za Serikali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya serikali katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17.

Sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama, na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Uwiano wa mitaji ya mabenki ikilinganishwa na rasilimali zao (*ratio of core capital to total risk weighted assets and off-balance sheet exposures*) ulikuwa asilimia 17.8 mwezi Desemba 2016, ikiwa juu ya kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 10.0. Hali ya ukwasi wa mabenki kiujumla imeendelea kubakia kwenye kiwango cha juu cha asilimia 42.4 ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 20. Wakati huo huo, uwiano wa mikopo chechefu, uliongezeka kufikia asilimia 9.5 mwezi Desemba 2016, kutoka asilimia 6.4 ya mwezi Desemba 2015.

Benki Kuu imeendelea na jitihada za kuimarisha usimamizi na udhibiti wa taasisi za fedha kwa kutoa miongozo mipya na inayokwenda na wakati katika kuboresha usimamizi na uendeshaji wa sekta ya fedha kwa viwango vya kimataifa. Aidha, Benki Kuu inaendelea pia kupitia mwongozo wa uwakala wa huduma za kibenki (*Banking Guidelines*) kwa lengo la kuboresha huduma hiyo ambayo imesaidia katika kupanua wigo wa utoaji huduma za kibenki kwa wananchi walio wengi zaidi na kwa gharama nafuu. Pia benki nyingi zimeendelea kushirikiana kwa karibu na makampuni ya simu katika kutoa huduma za kifedha na malipo kupitia simu za mikononi, hali ambayo imeendelea kupanua wigo wa utoaji huduma za kifedha kwa wananchi. Kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Malipo ya mwaka 2015, na miongozo yake, watoa huduma wapya ambao sio taasisi za kibenki wamepatiwa leseni ili waweze kutoa huduma za kifedha na malipo. Hadi kufikia mwezi Desemba 2016, Watanzania wapatao milioni 17.02 walikuwa watumiaji hai wa miamala kwenye mfumo wa malipo kupitia simu za mikononi.

**Zanzibar**

Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2016, pato la Taifa la Zanzibar lilikua kwa asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 8.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Kupungua kwa ukuaji wa pato la Taifa kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kasi ndogo ya ukuaji wa shughuli za ujenzi na mawasiliano. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 2.3 mwezi Novemba 2016, na kisha kuongezeka kidogo hadi asilimia 3.0 mwezi Desemba 2016, kutoka asilimia 9.3 mwezi Juni 2016. Hali hii ilitokana kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa bei za vyakula.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, mapato ya ndani ya serikali yalifikia shilingi bilioni 250.2, sawa na asilimia 6.1 zaidi

ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi hicho. Ongezeko la makusanyo ya mapato ya serikali limetokana na kuimarika kwa ukusanyaji wa kodi za uingizaji wa bidhaa (*import taxes*), kodi ya ongezeko la thamani (VAT), pamoja na ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa (*excise duties*). Jumla ya matumizi ilikuwa shilingi bilioni 282.1, sawa na asilimia 1.1 juu ya makadirio ya matumizi katika kipindi hicho; kati ya hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa ni asilimia 79.7 na matumizi ya maendeleo yalikuwa ni asilimia 20.3. Jumla ya misaada kutoka kwa wahisani ilifikia shilingi bilioni 22.1, ikilinganishwa na matarajio ya shilingi bilioni 5.4.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ilikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 35.4, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 40.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nchi za nje, pamoja na kupungua kwa uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, hususan mafuta.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2016/17

### *Malengo ya Sera ya Fedha*

Ili kufikia malengo ya serikali ya kuimarisha uchumi, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kutimiza malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 13.0;

ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 14.8;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 20.5; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2016/17***

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, serikali imeendelea na jitihada za kuongeza mapato na kuboresha usimamizi wa matumizi yake. Wakati huo huo, misaada ya fedha kwa ajili ya bajeti kutoka nje ya nchi imeendelea kupungua zikilinganishwa na viwango vya miaka iliyopita. Aidha, juhudi za kusimamia matumizi na makusanyo ya mapato ya serikali, pamoja na kuhamisha amana za mashirika ya umma kutoka benki za biashara kwenda Benki Kuu, kwa pamoja kulichangia upungufu wa ukwasi kwenye mabenki. Kufuatia mwenendo huu, Benki Kuu kupitia sera ya fedha ilichukua hatua za kuongeza ukwasi kwenye mabenki. Katika kipindi chote, Benki Kuu imeendelea kufuatilia kwa ukaribu na kuhakikisha hali ya ukwasi kwenye mabenki inaendelea kukidhi mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi, huku ikisimamia utulivu wa riba katika masoko ya fedha na mfumuko wa bei.

Pamoja na jitihada za Benki Kuu zilizolenga kuongeza ukwasi katika mabenki, wastani wa ukuaji wa fedha taslim (*reserve money*) ulibakia chini ukilinganishwa na malengo. Aidha, kuendelea kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya malipo kupitia simu za viganjani pamoja na kuimarika kwa utoaji huduma za kifedha nchini kulisaidia kwa kiasi kupunguza athari za ukuaji mdogo wa fedha taslim kwenye uchumi. Hali ya upungufu wa ukwasi hususan katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka 2016/17 ilijidhihirisha kupitia kuongezeka kwa riba katika soko la fedha baina ya mabenki (*interbank cash market rate*) na kufikia wastani wa asilimia 16.15 mwezi Septemba 2016, kutoka wastani wa asilimia 12.76 mwezi

Juni 2016. Aidha, hali ya ukwasi ilianza kuwa ya kuridhisha baada ya Benki Kuu kuchukua hatua mbalimbali, hali iliyowezesha kushuka kwa riba katika soko la fedha baina ya mabenki kuanzia mwezi Oktoba 2016 hadi mwezi Desemba 2016, na kubakia kwenye wastani wa asilimia 13.7.

Ukuaji mdogo wa wastani wa fedha taslim, ulisababisha kushuka kwa kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*extended broad money supply, M3*) kufikia asilimia 2.9 kwa mwaka ulioishia Desemba 2016, kutoka asilimia 12.5 ya mwaka ulioishia Juni 2016. Wakati huo huo, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 7.2 ikilinganishwa na asilimia 19.1. Kushuka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kumechangiwa pia na tahadhari zinazoendelea kuchukuliwa na mabenki katika kutoa mikopo kufuatia ongezeko la mikopo chechefu, hali ambayo pia imechangia kasi ndogo ya ukuaji wa ujazi wa fedha.

Thamani ya shilingi imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17, kutokana na msimamo wa sera ya fedha; pamoja na kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account*). Utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa matumizi na mapato ya serikali kuliwezesha kufikiwa kwa malengo yote ya vipengele vya sera ya fedha chini ya mpango maalumu kati ya IMF na Serikali kuhusu makubaliano ya utekelezaji wa Ushauri wa Kisera (*Policy Support Instrument*) kwa kipindi kinachoishia mwezi Desemba 2016.

***Matarajio ya Uchumi***

Uchumi unatarajiwa kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 7 mwaka 2016 na katika kipindi cha kati, ukichangiwa na utekelezaji wa sera

mbalimbali chini ya awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II*). Mpango huu umelenga kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika, ukarabati na ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa, ujenzi wa bandari na viwanja vya ndege, matarajio ya kuongezeka kwa uwekezaji kwenye ujenzi wa mitambo ya kuzalisha gesi, shughuli za uchimbaji madini, na kuanzishwa kwa maeneo mapya maalum ya shughuli za kiuchumi (*new special economic zones*).

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika viwango visivyozidi asilimia 10 katika siku zijazo na ndani ya lengo la asilimia 5. Hali hii itachangiwa na kutulia kwa bei ya nishati nchini inayotokana na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia katika uzalishaji wa umeme, muendelezo wa sera thabiti ya fedha na kibajeti, kuendelea kwa bei ndogo za mafuta katika soko la dunia, pamoja na kuendelea kuwepo kwa utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani. Hata hivyo, bado kuna viashiria vinavyoonesha kuwepo na uwezekano wa kuongezeka kwa mfumuko wa bei unaotokana na hali ya ukame pamoja na uwezekano wa kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje inatarajiwa kuimarika mwaka 2016/17 kufikia uwiano wa asilimia 4.0 ya pato la Taifa, kutoka asilimia 5.6 ya mwaka 2015/16. Hii inatokana na matarajio ya kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi, pamoja na kuendelea kupungua kwa uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi. Aidha, nakisi hiyo ya urari inatarajiwa kuongezeka katika kipindi cha kati kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoainishwa chini ya FYDP II.

*Mwenendo wa Sera ya Fedha Katika Nusu ya Pili ya 2016/17*

Kutokana na mwelekeo wa viashiria mbalimbali vya uchumi kwa siku za hivi karibuni, pamoja na mwenendo wa matumizi na ukusanyaji wa mapato ya serikali katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, malengo yalioainishwa katika Tamko la Sera ya Fedha ya mwezi Juni 2016 yanatarajiwa kufikia viwango vya chini kidogo kama ifuatavyo;

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 12.0;

ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.3;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 12.5; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2016/17, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya ukwasi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi yanafikiwa bila kuchochea mfumuko wa bei. Katika kuhakikisha ufanisi wa soko na utulivu wa viwango vya riba katika soko la fedha, Benki Kuu itaendelea kuboresha mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaolenga matumizi ya riba kama kiashiria cha mwelekeo wa sera ya fedha. Hatua hii ni pamoja na kuboresha mfumo wa namna mabenki yanavyokopeshana na kuufanya mfumo huo kuwa wa kielektroniki ili kuongeza ufanisi na uwazi baina ya mabenki (*electronic platform for interbank cash market operations*), pamoja na kufanya mapitio ya mfumo wa dhamana (*review of the collateral framework*) na kuendelea kukuza ufanisi katika mifumo ya malipo nchini.

## Hitimisho

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17, sera ya fedha ililenga katika kuhakikisha kuwa hali ya ukwasi inaendana na mahitaji halisi ya shughuli za kiuchumi. Benki Kuu kwa kutumia mbinu mbalimbali za sera ya fedha, iliendelea kuchukua hatua za makusudi katika kuongeza kiwango cha ukwasi katika mabenki ili kuchochea shughuli za kiuchumi nchini. Benki Kuu katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2016/17, itaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya ukwasi katika mabenki na kutumia mbinu za sera ya fedha kuhakikisha ukuaji wa ujazi wa fedha unawiana na lengo la mfumuko wa bei wa asilimia 5, pamoja na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 7, huku ikiendelea kuhakikisha utulivu wa riba katika masoko ya fedha.

Kuhusu utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2016/17, Benki Kuu itaendelea kushiriki kikamilifu katika masoko ya fedha, ili kuhakikisha utulivu wa riba za muda mfupi na upatikanaji wa ukwasi wa kutosha katika uchumi. Aidha Benki Kuu itaendelea kufuatilia mwenendo wa ukuaji wa uchumi na mfumuko wa bei na kuchukua hatua muafaka za kisera ili kuchangia katika utulivu wa uchumi.

Kutokana na matokeo mazuri ya utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17, pamoja na dhamira ya Serikali ya kuboresha mfumo wa ukusanyaji kodi na usimamizi wa matumizi ya serikali, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya Sera ya Fedha kwa mwaka 2016/17 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Kimepigwa Chapa na Identity Promotions Ltd